

## Die berühmte *Charité*

### Hospitali mashuhuri *Charité*

#### Muhtasari wa sarufi

##### Jikumbushe haya

##### Mwendesho wa vivumishi vya sifa

##### 1. Vivumishi vya sifa vinavyotangulia majina katika hali ya kike (f) na isiyo ya kike wala kume(n) kwenye umoja (singular)

Vivumishi vya sifa vinavyotangulia majina huongezewa kimalizikio kwa mujibu wa jina na hali ya jina hilo (gender) na iwapo lipo kwenye umoja (singular) au wingi (plural). Somo hili linatumia vivumishi vya sifa vinavyotangulia majina katika hali ya (f) na (n).

##### a) Baada ya *die/eine*

Baada ya kidhihirishi kikamilifu katika hali ya kike (feminine definite article) *die*, au kidhihirishi kisichokamilika *eine* katika uhusiano usiobadilika (nominative) na uhusiano wa moja kwa moja (accusative), kivumishi cha sifa huongezewa kimalizikio *-e*:

**die** berühmte *Charité*      **eine** freie Forschung

##### b) Baada ya *das*

Baada ya kidhihirishi kikamilifu katika hali ya (n) kwenye uhusiano usiobadilika (nominative) na uhusiano wa moja kwa moja (accusative), kivumishi cha sifa huongezewa kimalizikio *-e*:

**das** alte Haus

##### c) Baada ya *ein*

Baada ya kidhihirishi kisicho kikamilifu *ein* katika hali ya (n) kwenye uhusiano usiobadilika (nominative) na uhusiano wa moja kwa moja (accusative), kivumishi cha sifa huongezewa kimalizikio *-es*:

**ein** weltberühmtes Zentrum

##### 2. Vivumishi vya sifa vinavyotumiwa pamoja na majina katika hali ya wingi (plural nouns) bila ya kidhihirishi

Baada ya kidhihirishi kikamilifu katika hali ya wingi (plural definite article) *die* kwenye uhusiano usiobadilika (nominative) na uhusiano wa moja kwa moja (accusative), kivumishi cha sifa huongezewa kimalizikio *-en*.

Majina yanayotanguliwa na kidhihirishi kisicho kikamilifu kwenye hali ya umoja, huwa hayana kidhihirishi kwenye hali ya wingi. Vivumishi vya sifa vinavyotangulia majina kwenye hali ya wingi (plural nouns), katika uhusiano usiobadilika na uhusiano wa moja kwa moja, huongezewa kimalizikio *-e*, na *-en* katika uhusiano usiougwa moja kwa moja (dative).

	<b>Nominative (wingi)</b>	<b>Dative (wingi)</b>
<b>das</b> Gerät <b>der</b> Arzt <b>die</b> Klinik	moderne Geräte junge Ärzte moderne Kliniken	mit modern <b>en</b> Geräten von jung <b>en</b> Ärzten in modern <b>en</b> Kliniken

<b>Vimalizikio vya vivumishi vya sifa baada ya kidhihirishi kikamilifu</b>				
Umoja				Wingi
	(m)	(n)	(f)	
Nom.	<b>-e</b>	<b>-e</b>	<b>-e</b>	} daima <b>-en</b>
Acc.	<b>-en</b>	<b>-e</b>	<b>-e</b>	
Dat.	<b>-en</b>	<b>-en</b>	<b>-en</b>	

<b>Vimalizikio vya vivumishi vya sifa baada ya kidhihirishi kisicho kikamilifu</b>				
Umoja				Wingi
	(m)	(n)	(f)	
Nom.	<b>-er</b>	<b>-es</b>	<b>-e</b>	daima <b>-e</b>
Acc.	<b>-en</b>	<b>-es</b>	<b>-e</b>	daima <b>-e</b>
Dat.				daima <b>-en</b>

### **Vifungu vya maneno vilivyotumiwa katika mazungumzo**

etwas nicht genau wissen: Das weiß ich auch nicht so genau.

etwas vermuten: Ich kann das auch nur vermuten.

Und was bedeutet das?

Ein neuer Geist in alten Mauern.

Ja, so kann man sagen.

### **Habari kuhusu Berlin**

die *Charité*: *Charité* ni hospitali iliyo mashuhuri kote duniani. Hospitali hiyo ilijengwa mwanzoni mwa karne ya 18 kuhudumia magonjwa mabaya ya kuambukiza. Kwa kadiri miaka miya moja, mpaka 1933, *Charité* kilikuwa kituo cha utafiti sayansi. Mwenendo mrefu huu umekuwa ukiendelezwa na madakitari vijana mpaka leo.

*Andreas, Ex na Dr. Thürmann wako Berlin ya Mashariki. Wamesimama mbele ya Charité – hospital mashuhuri ambako Dr. Thürmann aliwabi kufanya kazi. Wanalizungumzia jina la hospitali hiyo, pia wanataka kujua asili ya jina hilo.*

Ex: Schau mal, da oben, die großen Buchstaben.  
(anasoma kwa sauti) *Cha – ri – té.*

Andreas: *Charité*, Ex, *Charité*.  
 Dr. Thürmann: Ja, das ist die berühmte *Charité*, ein weltbekanntes Krankenhaus. Da habe ich auch mal gearbeitet.  
 Andreas: Warum heißt die *Charité* so?  
 Dr. Thürmann: Das weiß ich auch nicht so genau, ich kann das nur vermuten: Die *Charité* ist ja sehr alt, schon fast 300 Jahre. Und damals, 1710, als man die *Charité* gründete, waren ja viele Franzosen in Berlin.  
 Ex: *Charité* ist also französisch?  
 Andreas: Ja.  
 Ex: Und was bedeutet das?  
 Andreas: Barmherzigkeit.  
 Ex: Wie bitte?  
 Andreas: Mitleid haben, den Kranken helfen.

*Dr. Thürmann anasimulia historia ya Charité.*

Andreas: Und warum ist die *Charité* so berühmt?  
 Dr. Thürmann: Die *Charité* war ein weltbekanntes Forschungszentrum: Man hat schon sehr früh komplizierte Operationen gemacht. Aber nicht nur das: Es gab eine freie Forschung, sehr gute Ärzte haben hier gearbeitet – und mehrere Nobelpreise erhalten.  
 Andreas: Aber jetzt sieht das alles ziemlich alt aus.  
 Dr. Thürmann: Natürlich! In der Nazizeit mußten die jüdischen Ärzte gehen, und später sind viele Ärzte in den Westen gegangen. Es gab moderne Geräte, eine gute Medizin – aber man forschte nicht mehr so viel.  
 Andreas: Und heute?  
 Dr. Thürmann: Ich habe gehört, daß es eine Initiative von jungen Ärzten gibt: Sie wollen dieses traditionsreiche alte Haus wieder beleben.  
 Andreas: Ein neuer Geist in alten Mauern?  
 Dr. Thürmann: Ja, so kann man das sagen.

## **Maneno na vifungu vya maneno**

---

der Buchstabe, die Buchstaben	herufi
weltbekannt	mashuhuri kote duniani
das Krankenhaus	hospitali
vermuten	-kisia, -fikiria
fast 300 Jahre alt	karibia miaka 300
gründen	kujenga, kuunda, kuasisi
die Barmherzigkeit	huruma
Mitleid haben	kuwa na huruma (-onea huruma)
das Mitleid	huruma
der Kranke, die Kranken	mgonjwa, wagonjwa
das Forschungszentrum	kituo cha utafiti wa sayansi
kompliziert	-gumu, -kanganya
die Operation	upasujaji, operesheni

aber nicht nur das  
freie Forschung  
die Forschung  
mehrere Nobelpreise  
der Nobelpreis  
erhalten  
die Nazizeit  
jüdisch  
moderne Geräte  
modern  
das Gerät  
die Medizin  
forschen  
die Initiative  
traditionsreich  
beleben  
neuer Geist in alten Mauern  
(*msemo*)

na siyo hivyo tu  
utafiti huru wa sayansi  
utafiti wa sayansi  
tuzo nyingi za Nobel  
tuzo la Nobel  
-pata, -pokea, -shinda  
wakati wa utawala wa Wanazi  
Kiyahudi  
vyombo, vifaa vya kisasa  
-kisasa, -kimambo leo  
chombo, kifaa  
utibabu, matibabu  
-fanya utafiti wa sayansi  
juhuri  
-enye mila ndefu (kubwa)  
-fufua  
upepo wa mabadiliko

## Mazoezi

---

- 1** Soma tema maandishi (text) katika somo hili, kisha tafuta maneno yenye kufanana katika lugha nyingine. Yaandike maneno hayo hapo chini.
- 
- 

- 2** Kamilisha kwa ufupi maelezo ya hapo chini juu ya historia ya *Charité*.

### *Charité*

sehr alt: \_\_\_\_\_ gegründet: \_\_\_\_\_

Name bedeutet: \_\_\_\_\_

war: \_\_\_\_\_

man machte \_\_\_\_\_ es gab \_\_\_\_\_

mehrere \_\_\_\_\_

Nazizeit: \_\_\_\_\_

später: \_\_\_\_\_

heute: \_\_\_\_\_

**3 Chagua vivumishi vya sifa vinavyofuatana na majina (nouns) hapo chini, kisha tunga vifungu vya maneno kufuatana na mfano uliotolewa. Usisahau kutumia kidhihirishi kinachofaa.**

Zentrum Operation Forschung Ärzte Geräte Haus Geist Mauer  
modern gut alt weltbekannt frei kompliziert neu jüdisch jung

Beispiel

Zentrum – modern: das moderne Zentrum, ein modernes Zentrum,  
in einem modernen Zentrum

**4 Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia vivumishi vya sifa kutoka kisanduku hapo chini. Usisahau kuongezea kimalizikio kinachofaa.**

1. Die *Charité* war ein \_\_\_\_\_ Forschungszentrum.
2. Man hat schon sehr früh \_\_\_\_\_ Operationen gemacht.
3. Es gab eine \_\_\_\_\_ Forschung.
4. Hier haben sehr \_\_\_\_\_ Ärzte gearbeitet.
5. In der Nazizeit mußten die \_\_\_\_\_ Ärzte gehen.
6. Es gab \_\_\_\_\_ Geräte.
7. Es gibt eine Initiative von \_\_\_\_\_ Ärzten.
8. Sie wollen dieses \_\_\_\_\_ Haus wieder beleben.
9. Ein \_\_\_\_\_ Geist in \_\_\_\_\_ Mauern.

modern alt jung kompliziert jüdisch weltbekannt gut alt frei neu